Mkulima Mbunifu

Jarida la Kilimo Endelevu Afrika Mashariki

Toleo la 124| Februari 2023

Yaliyomo

Namna ya kuanza kilimo hai 2
Uzalisha wa chakula salama 8



Mnyororo wa thamani 10
Soko la mazao ya kilimo 12

# Taarifa: Mkulima Mbunifu ni mara moja kwa miezi miwili tangu sasa




***Mwaka umeanza ukiwa na baraka tele na habari njema kwa wakulima na wasomaji kwa ujumla. Kuanzia mwezi huu jarida lako ulipendalo la Mkulima Mbunifu (MkM) litakuwa likichapishwa na kuletwa kwako kila baada ya miezi miwili.***

Tangu jarida hili lilipozinduliwa mwezi Julai 2011, limekuwa likichapishwa na kusambazwa kwa wakulima kila baada ya miezi miwili. Hata hivyo sababu ilikua ni kujenga msingi imara wa utoaji elimu na taarifa kwa wakulima.

Tangu mwaka 2014 hadi mwaka jana 2022, kipindi cha miaka nane, Jarida lilikua likichapichwa mara moja kwa kila mwezi na tumekua na wasomaji wengi ingawa kumekua na changamoto ya kutopata mrejesho na baadhi ya wasomaji kutopokea kwa wakati.

Kwa kuzingatia hilo, jarida litatolewa mara moja kila baada ya miezi miwili na litawafikia wakulima ambao tunataarifa zao kamili. Hii itatusaidia kuwa na mawasiliano ya mara kwa mara na wasomaji wa jarida. Pia, tumeongeza kurasa nne ili kutoa nafasi ya waandishi kupambanua taarifa zaidi.

Wakulima wanashauriwa kufuatilia katika masanduku yao ya posta, vikundi, taasisi zilizopo chini ya kanisa, mashirika ya kijamii, na taasisi zisizo za kiserikali ambazo huwa zinasambaza majarida haya, ili kuhakikisha kuwa hawakosi nakala kila toleo. Lakini, ukikosa nakala iliyochapishwa, usikate tama, unaweza kupata nakala yako kupitia kwenye tovuti yetu.

Endapo wewe ni mmoja wa wakulima na wafugaji wanaokua na kufanya shughuli zao kwa ufanisi, tutafurahi kusikia kutoka kwako ili tuweze kuwashirikisha wakulima wengine, nao waweze kupiga hatua kwa kujifunza kutoka kwako. Tunaamini kuwa wakulima wanaposhirikishana uzoefu, ni njia rahisi ya kila mmoja kujifunza kutoka kwa mwingine.

Somo ambalo umeweza kujifunza kutoka katika shughuli zako za kilimo na ufugaji, ni njia nzuri ya kuwasaidia wengine kutatua matatizo yanayowakabili katika shughuli zao.

Hivyo, itawasaidia kusonga mbele. Kwa pamoja, tuwasaidie wengine, usiwe mchoyo, wasiliana nasi ili tukutembelee na kuwapatia wengine yale uliyo nayo.

## *Mpendwa Mkulima*

*Heri ya mwaka mpya wa 2023. Ni jambo la kushukuru na kufurahia kuwa tumeweza kuwa tena katika mwaka huu. Ni wazi kuwa kila mmoja pia ameanza akiwa na mipango mipya, au kuendeleza ile ambayo alikwisha iweka tangu mwaka uliopita.*

*Kwako wewe ambae hujaweka mipango, hujachelewa weka mipango thabiti itakayokuwezesha kufikia malengo na yale yote unayotamani kuyafanya kwa mwaka huu wa 2023.*

*Ni dhahiri kuwa bila mipango thabiti, shughuli za kilimo na ufugaji haziwezi kufanikiwa kwa asilimia kubwa. Sambamba na kuweka mipango thabiti, kumbuka kuwa, bila kuwa na taarifa sahihi, ni vigumu pia kuweza kufanya jambo lenye tija. Hii ndiyo sababu wachapishaji wa jarida hili la wakulima - Mkulima Mbunifu, tumeona uhitaji mkubwa wa wakulima na wafugaji kupata taarifa sahihi.*

*Pamoja na hayo ni wazi kuwa bila ushiriki wako kikamilifu, mpango huu hautaweza kuwa na ufanisi kama ilivyokusudiwa. Hii ikiwa na maana kuwa uhakikishe kuwa taarifa hizi zinakufikia kila wakati na uzitumie ipasavyo katika kuboresha maisha yako na ya jamii inayokuzunguka kwa ujumla.*

*Pia, litakuwa ni jambo jema na lenye heshima unapopata jarida hili la Mkulima Mbunifu, uwashirikishe wengine, pia unaweza kuwasiliana nasi kwa maelezo zaidi.*

*Tunaendelea kusisitiza kututumia taarifa kamili za kila mwanakikundi, jina, mme/mke namba ya simu, mahali alipo na anuani ya posta au barua pepe ili uendelee kunufaika na mafunzo yanayoandikwa humu.*

Kwa uhitaji wa jarida hili wasiliana nasi kwa kutupigia simu au kwa anwani kwa kupitia barua pepe, facebook, tovuti na sanduku la posta kama zilivyoonyeshwa hapa;

+255 717 266 007
http://www.facebook.com/mkulima_mbunifu
http://twitter.com/mkulima_mbunifu
https://www.instagramu.com/mkulima_mbunifu
mkulimambunifu.org
theorganicfarmer.org
infonet-biovision.org

Wasiliana na *MkM*,
S. L. P 14402, Arusha,
Simu: 0717 266 007, 0762 333 876,
Barua pepe:
info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org


# Fahamu kuhusu kilimo hai na namna ya kuanza

***Kwa kawaida viumbe hai vyote ni vya asili. Fikra na mitazamo juu ya kilimo hai inaonekana kama vile viumbe hai wana sehemu yao maalumu tangu miaka mingi iliyopita. Hii inajumuisha viumbe wadogo wadogo waliopo ardhini, kwenye mimea, wanyama pamoja na binadamu mwenyewe.***

**Erica Rugabandana**

Mfumo wa kilimo hai umetelekezwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko katika sekta ya viwanda, ongezeko la watu na mahitaji makubwa ya chakula katika nchi zilizoendelea kwa karne nyingi na zinazoendelea hivi sasa.

Kilimo hai kimejaribu kuangalia na kupata picha nzima ya mazingira siyo tu aina moja ya wadudu wanaweza kuuliwa, lakini kilimo hai kimejaribu kuweka sawa shughuli za kilimo kwa njia za asili za uzalishaji wa mazao ya chakula na mazao mengine kwa mzunguko wa kiasili.




### Rutuba ya udongo, mimea, binadamu

Kilimo hai ni lazima kiwezeshe na kiongeze rutuba ya udongo, afya ya mimea, wanyama na binadamu. Udongo ni nguzo muhimu katika maisha ya viumbe wote kwa ujumla. Udongo ulioharibiwa hauwezi kuzalisha chakula kizuri pia malisho ya kutosha kwa ajii ya mifugo. Ili kuweza kupata chakula cha kutosha kwa ajili ya binadamu na malisho ya wanyama, ni lazima kuboresha rutuba ya udongo. Afya ya binadamu na wanyama inaenda sambamba na umuhimu na ubora wa udongo.

### Mashamba ni sehemu ya ikolojia

Kilimo hai ni lazima kitegemee mzunguko na mfumo mzima wa ikolojia. Mambo hayo hayawezi kutenganishwa lazima yapokelewe katika hali zote na kukubalika katika nyanja za kilimo, kijadi na kiutamaduni.

### Usawa katika mahuusiano yote

Wakulima wanaofanya kilimo hai wanahitaji kuona kuwa wanashirikiana katika maisha ya ulimwengu huu na viumbe hai wote, pamoja na hayo binadamu na wanyama wanatakiwa kupata nafasi yao ya kuwa na afya njema na furaha. Hii inajumuisha usawa katika ngazi zote na kwa wakulima, wafanyakazi na wafanyabiashara. Kilimo hai kinalenga kuhakikisha ubora wa maisha ya kila mtu, na kuchangia ukombozi wa chakula na kupunguza umaskini. Uasili na mazingira ni lazima vitunzwe kwa ushirikiano na ikolojia.

### Uangalifu- Tahadhari

Wakulima wa asili hutekeleza majukumu yao kama watumiaji makini wa ardhi. Ardhi kwa ajili ya kilimo na miundo mbinu mingine kama vile vyanzo vya maji, ni lazima vitunzwe katika hali nzuri, kwa ajili ya kizazi kijacho. Watu na wanyama ni lazima watunzwe na kuangaliwa kwa umakini ili kihakikisha afya zao zinaendelea kuwa salama. Teknolojia ya kisasa, pamoja na njia za kiasili ni lazima zichunguzwe na kuangaliwa kwa kufuata taratibu za kiasili. Tahadhari za kuzuia ni lazima zizingatiwe ili hatari zinazoweza kujitokeza zidhibitiwe na maamuzi yazingatie thamani na mahitaji ya viumbe wote wanaoweza kuathiriwa.

### Mbinu za kilimo hai kwa ufupi.

### Kilimo cha asili

Mfumo wa kilimo cha asili unajumuisha muundo wa kilimo cha jadi ambao umekuwa ukitumika kwa karne nyingi. Kwa kawaida huzingatia matumizi mazuri ya miundo mbinu inayopatikana na njia za kienyeji, hali ya ikolojia na mahusiano thabiti. Ikiwa mbinu za kijadi zikifuatwa, mbali na mabadiliko ya hali halisi, zinaweza kusababisha madhara, vinginevyo ni lazima zirekebishwe. Mfano mbinu za kiasili ya kufyeka na kuchoma moto, hili si tatizo endapo ni sehemu ndogo tu ya ardhi ndiyo inayotumika kwa kilimo. Mbinu hiyo hiyo iinaleta uharibifu wa misity pamoja na arddhi, pale tu kunapokuwepo ongezeko la watu, hivyo kupunguza utunzaji wa ardhi.

### Kilimo mchanganyiko

Mtindo wa kilimo mchanganyiko unajumuisha faida za mbinu zote zinazotumika katika kilimo. Hupunguza na kuepuka madhara yanayotokana na kilimo cha kisasa kwa kujumuisha mbinu za kilimo hai, kwa kupunguza matumizi ya mbolea za viwandani na kemikali, na kuchagua kwa uangalifu viuatilifu. Katika nchi nyingi hii inaonekana kuwa njia sahihi ya kurekebisha madhara yanayotokana na kilimo cha kisasa.




### Kilimo hai kwa vitendo: Mtazamo

### Virutubisho hai

Mbolea zisizo za asili hazitumiki katika kilimo hai. Virutubisho vya asili vinavyotokana na mimea hutumika kurutubisha udongo. Kuongeza rutuba kwenye udongo huchukuliwa kama nguzo muhimu. Mbolea za asili hutumika kuboresha au kushikilia rutuba ya udongo, kwa kuongeza mbolea inayotokana na mifugo, mbolea vunde, na kuacha mabaki ya mazao shambani yatumike kama matandazo. Mbolea za asili huwa na virutubisho kama vile N,P na K. virutubisho hivi hupatikana wakati viumbe hai wadogo walioko kwenye ardhi wanapovunja vunja mbolea hizo wakila.

- Nitrojeni (N): Chanzo kizuri cha asili ya nitrojeni kwa mimea kinatokana na mkojo wa wanyama na aina zote za samadi za wanyama. Mbolea zinazotokana na mimea na wanyama hutoa nitrojeni nzuri kwa mimea. Mimea jamii ya mikunde na mbolea vunde ni chanzo kizuri cha asili kuweza kuipatia mimea nitrojeni.
- Fosiforasi (P): njia za asili za kupata fosiforasi ni kupitia mbolea ya miamba, mbolea ya kuku na wanyama wengineo.
- Potashiamu (K): njia za asili za kupata potasiamu ni majivu, samadi ya mbuzi, kondoo na mifugo mingine.

### Udhibiti wa wadudu na magonjwa kwa njia za asili

Kulima kwa mzunguko ni njia kuu ya kuweza kudhibiti wadudu na magonjwa. Mazao yanayostahimili aina fulani ya wadudu na magonjwa ni lazima yapewe kipaumbele. Kilimo hai ni lazima kisaidie ustawi wa wadudu wenye faida pamoja na wanaosaidia kula visumbufu vya mazao, kwa kuwa husaidia kufanya mimea kuwa na afya na kuiwezesha kukabiliana na wadudu na magonjwa.

### Udhibiti wa magugu

Udhibiti wa magugu katika kilimo hai hutegemea mzunguko wa mazao, kupanda mimea inayotambaa, na kutumia mbolea vunde sehemu ambayo kuna uhaba wa mimea inayotambaa, pamoja na kufunika ardhi kwa kutumia aina tofauti za matandazo (hii ni pamoja na kutumia plastiki). Kupalilia mapema, kuandaa ardhi mapema na kuacha mabaki ya mazao shambani, husaidia kupunguza wingi wa magugu. Kupalilia kwa mikono au jembe, au kufyeka na kuacha magugu shambani kama matandazo ni muhimu kwa mazao mengi.

### Ufugaji wa asili

Mifugo ni moja ya sehemu muhimu sana katika kilimo hai. Wanyama hutoa samadi ambayo hutumika kama mbolea. Mimea ya malisho inaweza kutumika katika mzunguko wa mazao. Nyasi na malisho ya jamii ya mikunde ni malisho bora kwa wanyama wanaocheua lakini pia husaidia kujenga udongo, kuupatia nitrojeni, na ni mazuri katika kufanya mzunguko wa mabaki ya mazao.

Afya ya wanyama, inapewa kipaumbele kwa kuwa kuzuia magonjwa ni moja ya nguzo muhimu katika kilimo hai. Afya ya mifugo katika kilimo hai, huimarishwa kwa kuzingatia kuwa na mbegu bora, kuwa na malazi safi na makavu pamoja na nyumba bora, kuchunga pale inapowezekana, pamoja na ulishaji unaozingatia upatikanaji wa virutubisho vyote na kwa kiwango kinachojitosheleza.




### Ni faida gani zinazoweza kutarajiwa kutokana na kilimo hai?

- Kilimo hai huongeza rutuba kwenye udongo kwa muda mrefu. Udongo hai una kiasi kikubwa cha virutubisho vinavyotokana na uozo wa malighafi za asili. Pia huongeza uwezo wa ardhi kuzalisha, kuhifadhi maji kwa muda mrefu na kukabiliana na ukame.
- Kilimo hai hakihitaji kuwekeza gharama kubwa. Kilimo hai hutumia miundo mbinu inayopatikana kirahisi hivyo kumuepushia mkulima mdogo gharama za pembejeo za viwandani.
- Kilimo hai hakimuweki mkulima pamoja na familia yake katika athari ya kupata magonjwa yanayotokana na matumizi ya kemikali na mbolea za viwandani.
- Kilimo hai kinajumuisha tafiti za kisayansi na kilimo cha kijadi katika kilimo endelevu.
- Hata kama kanuni za kilimo hazijazingatiwa ipasavyo, na hata kama hakuna soko la mazao ya kilimo hai yaliyozalishwa, mazao na bidhaa zake yanaweza kupatikana, na shamba pia hufaidika kwa kutumia mbinu za kilimo hai.

***Kwa maelezo zaidi Unaweza kuwasiliana na Mkulima Mbunifu kwa simu namba +255 0717266007 au kwa barua pepe info@mkulimambunifu.org***

*Mkulima Mbunifu* ni jarida huru kwa jamii ya wakulima Afrika Mashariki. Jarida hili linaeneza habari za kilimo hai na kuruhusu majadiliano katika Nyanja zote za kilimo endelevu. Jarida hili linatayarishwa na *Mkulima Mbunifu*, Arusha, ni mojawapo ya mradi wa mawasiliano ya wakulima unaotekelezwa na Biovision (www.biovision.ch) kwa ushirikiano na Sustainable Agriculture Tanzania (SAT), (www.kilimo.org), Morogoro. Jarida hili linafadhiliwa na Biovision Foundation

icipe — African Insect Science for Food and Health
biovision

**Wachapishaji:** African Insect Science for Food and Health (ICIPE), S.L.P 30772 – 00100 Nairobi, Kenya, Simu: +254 20 863 2000, icipe@icipe.org, www.icipe.org

**Mpangilio:** Cathbert Msemo 0652 731 123
**Mhariri:** Erica Rugabandana
**Mhariri Msaidizi:** Flora Laanyuni
**Anuani:** *Mkulima Mbunifu*
Sakina, Majengo road, (Elerai Construction Block)
S.L.P 14402, Arusha, Tanzania
Ujumbe mfupi pekee: 0785 496 036, 0766 841 366
Piga simu: 0717 266 007, 0762 333 876
Barua pepe: info@mkulimambunifu.org
www.mkulimambunifu.org

Toleo la 114 | Februari 2023

# Vidokezo vya kuanzisha biashara ya ufugaji wa wanyama




***Ufugaji ni utunzaji na uzalishaji wa mifugo kwa madhumuni ya kilimo, ikiwa ni pamoja na chakula na bidhaa zingine zitokanazo na mifugo. Ikifanywa ipasavyo, ni shughuli yenye uwezo mkubwa ya kumkwamua mkulima na kumpa mapato ya kutosheleza mahitaji ya kila siku.***

**Frank Ademba**

Wengi wa wakulima wadogo huunganisha ufugaji na kuzalisha mazao, ingawa baadhi ya wakulima huzingatia ufugaji pekee, ili kuwawezesha kupata fursa ya kufuga aina moja au mbili kwa ufasaha.

Wafugaji wanatumia rasilimali kama vile nyasi, maji na kadhalika kuwawezesha wanyama kuzalisha. Ufugaji sio tu kuangazia myama bali pia inahusisha mchakato mzima wa kuzalisha rasilimali zinazotumika katika ufugaji.

Bidhaa kutokana na ufugaji kama vile nyama ina uhitaji mkubwa katika soko kwa kuwa na manufaa mengi kiafya. Ni biashara yenye faida kubwa na inaweza pia kuwa na kazi nyingi. Kwa hivyo, ni muhimu kuangalia na kujua chaguo bora kwako ili kuweza kufanya ambayo yatakuletea faida zaidi.

Kwa mfano, hutapata faida nzuri katika hali ambayo unazingatia ufugaji wa nguruwe pekee katika eneo ambapo watu wengi wanapendelea kula kuku au mbuzi. Uelewa wa soko unalolenga unachangia pakubwa katika ufanisi wa biashara ya ufugaji.

Unapofikiria kuingia katika sekta ya ufugaji hapa Tanzania, tunakupa vidokezo vya kuzingatia unapojiandaa kufanya ufugaji wenye mafanikio. Na hapa tunatumia mtazamo wa kibiashara kwa sababu lengo kuu ni mkulima kuinua hali yake kwa kuzalisha zaidi na kuuza zaidi.

## Nini Kusudi Lako?

Huwezi kufanikisha ufugaji kama hujui na huelewi lengo lako vizuri. Kujua sababu ya kufanya shughuli za ufugaji ni muhimu sana kwa sababu husaidia kujua nini unataka na jinsi gani unaweza kufikia lengo lako. Ikiwa unapanga kuingia katika ufugaji wa wanyama, wa nyama na bidhaa za maziwa, basi ng'ombe au mbuzi wanaweza kuwa chaguo bora zaidi.

Kuelewa kusudio lako husaidia kuelezea kile unachotaka. Hii ni muhimu sana katika kuanzisha ufugaji kwa sababu unachochagua ndicho kitakachoamua vifaa vinavyohitajika.

Kwa ajili ya kuendesha biashara ya uzalishaji wa maziwa, inahusisha kufuga mifugo hasa kwa ajili ya bidhaa za maziwa, na biashara ya uzalishaji wa nyama inahusisha ufugaji wa mifugo hasa kwa ajili ya matumizi ya nyama. Hivyo, huwezi kuwanunua ng'ombe wa nyama ili kuzalisha maziwa. Hapo, utapoteza au mapato yako yatakuwa ya chini mno.

Tunarudia kwamba, kuna aina nyingi za uzalishaji katika ufugaji. Kwa mfano, unaweza kuwekeza katika ng'ombe kwa ajili ya uzalishaji wa maziwa na/au kutengeneza na kuuza jibini, mkulima mwingine anaweza kuwekeza kwenye kuku wa nyama au mayai, mwingine kwa nguruwe na kadhalika. Hapa Tanzania, kila mkoa una nguvu na udhaifu wake; mjasiriamali katika nyanja hii ya ufugaji anapaswa kushauriana na idara ya mifugo katika wilaya yake ili kutengeneza mkakati ambao utafanya kazi vyema katika eneo husika.

## Tafuta Mahali

Unazalisha wapi? Kupata eneo kunategemea ikiwa unaingia katika biashara kubwa au ndogo; yaani, unatazamia kuwafuga wanyama wengi au wachache. Hii itasaidia kuamua eneo bora kwa biashara yako. Ingawa, unaweza kuanza na eneo dogo na wanyama wachache kisha ukapanua biashara yako kwa utaratibu, hatua kwa hatua kulingana na mapato yako na pia mtaji unaopatikana.

Sambamba na hili, ni muhimu kujua ukubwa wa ardhi unayohitaji kwa uzalishaji wa mifugo yako. Kwa mfano, utahitaji eneo dogo kuzalisha kuku wa mayai kama unanunua chakula cha kuku kutoka madukani. Lakini, kama unapanga kuzalisha malighafi kama vile mahindi, soya, na kadhalika, na kutengeneza chakula nyumbani basi lazima uongeze ukubwa wa shamba kulingana na idadi ya kuku unaowafuga. Vivyo hivyo, kiasi cha ardhi kinachotumika kwa ng'ombe ni tofauti na ile inayotumika kwa ufugaji wa sungura.

Ni muhimu pia kuwa karibu na miundo mbinu muhimu kama vile maji, barabara na umeme. Hakikisha barabara sio mbovu kiasi kwamba italeta shida kubwa kwako kusafirisha mifugo au bidhaa yako kwenda sokoni. Hata hivyo, tunasema anza au fanya ulipo!




## Ulishaji Sahihi

Kulisha ni muhimu sana katika ufugaji wa mifugo, hivyo kama unajishughulisha na ufugaji wa kondoo, ng'ombe, mbuzi, na mwanyama wengine wanaokula nyasi, inashauriwa kupanda nyasi shambani mwako au karibu na eneo lako kwa sababu itasaidia kupunguza gharama zinazoweza kutokea katika utoaji wa chakula na virutubisho vingine.

Ulishaji unajulikana kuwa moja ya sababu muhimu kwa ufugaji wa mifugo wenye mafanikio kwa sababu wakilishwa vizuri, watazalisha inavyopaswa. Kulisha mifugo vizuri haimaanishi kulisha kupita kiasi, lakini inamaanisha kuwapa chakula kinachofaa na kinachotosheleza mahitaji.

Kulisha mifugo kunahitaji maarifa, ujuzi na uzoefu mwingi ili kuweza kulisha inavyotakiwa. Ni muhimu sana kuelewa aina mbalimbali za vyakula vinavyoweza kulishwa kwa mifugo, na kisha kujifunza jinsi vyakula mbalimbali vinavyoweza kuunganishwa pamoja ili kutengeneza mgao sawia kwa wanyama.

Ukweli ni kwamba, unaponunua mnyama mzuri kisha unashindwa kumlisha hiyo ni hasara ama kazi isiyo na faida.

Hivyo, tuwekeze katika ulishaji, hasa kuelewa ni nini tunawalisha mifugo, wanahitaji virutubisho gani kwa viwango gani, na inagharimu kiasi gani. Hapa ndio inatofautisha yule mkulima atapata faida na yule wa hasara.

## Fahamu kuhusu Soko

Kufikiria swala la soko mwanzoni, ni muhimu sana, kwa sababu sio tu kuelewa upatikanaji wa soko bali pia soko hili litafikiwa vipi? Kuzingatia tu kuzalisha bidhaa za ubora wa juu haitoshi, lakini ni muhimu kujua utakavyouza bidhaa zako; na wapi unaweza kuuza bidhaa.

Elewa nyakati ambazo soko huwa na bei bora zaidi ili kuendana na mzunguko wa uzalishaji. Utakuwa unatabasamu wakati wengine wananung'unika. Kumbuka, unaanza na kufikiria juu ya soko kwa sababu ndio itaamua unafuga nini na wapi.



## Tenga Muda

Ufugaji wa mifugo unahitaji kujitolea sana. Wanyama wengi wanahitaji kulishwa na kupewa maji kila siku. Kuchunguza mara kwa mara kiwango cha maji ni muhimu sana, pia ni lazima kama unapanga kuanzisha ufugaji. Ukaguzi wa kila siku wa mifugo wako ni mojawapo ya njia bora za kuzuia majeraha, hivyo, lazima uwe karibu.

Ukitaka kuwa na ufugaji wenye faida na mafanikio unahitaji kuwekeza muda wako ili kuwatunza mifugo ipasavyo.

Ikiwa umeajiriwa ama unapanga kuondoka nyumbani kwa muda mrefu, unahitaji kupata mtu ambaye atasaidia katika kuangalia na kuwatunza wanyama wako. Lakini hii itategemea mapato yako na ufugaji wenyewe.

### Tueleze Malengo Yako

Katika matoleo mengine ya gazeti hili, tutaangazia mahitaji maalum kwa kila aina ya ufugaji wa mifugo ili kuhakikisha tunatembea nawe hatua kwa hatua katika kuanzisha na kukuza biashara yako. Ukiwa na swali au ungependa aina fulani ya ufugaji liangaziwe, wasiliana na MkM, na utujulishe hitaji lako ili tuendelee kushirikishana mafunzo.

Ufugaji unachangia maendeleo

Biashara za ufugaji hupata pesa kupitia uuzaji wa mifugo yao iliyokuzwa na rasilimali zingine ambazo mifugo inazalisha.

Kwanza, uzalishaji wa mifugo huongeza upatikanaji wa vyakula vya asili vya wanyama ambavyo ni vyanzo vya protini na virutubishi vingine vinavyohitajika na mwili kwa viwango vidogo, na ni muhimu kwa watu wenye afya. Kaya zenye mifugo hutoa lishe bora kwa wanafamilia wote; wanakula nyama, mayai, na vyanzo vingine vinavyotokana na wanyama.

Pili, uzalishaji wa mifugo huchangia maendeleo ya kiuchumi katika ngazi ya kaya na jamii kupitia kazi hii ya kipato na kuweka akiba. Mnyama anayetembea ni mali, rasilimali inayotumika kuzalisha zaidi, na ni akiba inayoweza kubadilishwa kuwa pesa taslimu sokoni, na kutumika kugharamia mahitaji tofauti ya familia, mfano, kulipa karo shuleni.

Tatu, kuna kipato kwa wafanyabiashara wa bidhaa na huduma zinazotumika na wafugaji. Daktari wa mifugo anapata sehemu yake, muuza chakula cha mifugo dukani, afisa ugani, wasimamizi serikalini, watafiti, mchinjaji, mchuuzi na wengine wengi wanachuma kipato kutokana na ufugaji.

Nne, na kutokana na hayo, nafasi ya uzalishaji wa mifugo katika maendeleo ya taifa ni kubwa.

Tafuta nafasi yako na ujikite, ujenge na upate sehemu yako ya kipato cha sekta hii!

# Mkulima atumia kilimo hai kujiendeleza baada ya kustaafu

***"Naitwa Felister Mangalu (64) mkulima wa kilimo hai. Nilikua mfanyakazi wa serikali na nikastaafu mwaka wa 2019. Kabla ya kustaafu nilikuwa nikijiuliza maswali kuhusu nini nitafanya ili kuendelea kujikimu kimaisha endapo muda wangu wa ajira ukiisha.***

**Erica Rugabandana**




Najua hili ni swali ambalo watu wengi hujiuliza wakiwa na sababu kama zangu. Hata hivyo, najua tumejaliwa vipawa mbalimbali na tuna uwezo tofauti tofauti. Wakati wa kustaafu ama mtu anapofikiria kitu cha kufanya, uamuzi utategemea sana kile alichozoea kufanya, ujuzi na pia rasilimali zinazopatikiana kwake.

Kwa upande wangu, nilisomea stashahada ya sayansi ya mimea, ambapo shahada ya uzamili nilisoma kuhusu kilimo endelevu. Kwa hivyo, niliamua kujitosa katika ulingo wa kilimo. Hii ndio kazi ambayo niliona ninaweza kuimudu, ingawa nilikua na hofu kama nitaweza kuisimamia vizuri ili nipate faida."

MkM ilifanikiwa kumjua mama Mangalu kupitia soko la kilimo hai la Mesula ambapo wakulima wa kilimo hai hupeleka mazao ya mbogamboga kuuza. Mama huyu ambaye ni mkulima wa kilimo hai pia ni mnufaika wa jarida la Mkulima Mbunifu.

Mkulima Mbunifu iliamua kumfuatilia nyumbani ili kuangalia shughuli anazofanya kujifunza kutoka kwake ili kuwafikishia elimu wakulima wengine. Mama Mangalu anasema kwamba aliamua kufanya kilimo hai baada ya kutambua kuna faida katika kilimo hiki tofauti na kilimo cha kawaida ambacho kinahusisha matumizi ya mbolea za viwandani na dawa za kemikali, na hii hufanya gharama ya uzalishaji kuwa juu hasa kwa wakulima wadogo wenye mapato ya chini.

Mama huyu anaongeza kuwa, kwake yeye, afya na usalama wa chakula ni jambo la msingi kwani tunahitaji kula kila siku na sio tu kushiba bali kupata virutubisho muhimu kwa ukuaji na kuhakikisha tunakula chakula ambacho hakijumuishi vitu au mabaki ambayo ni hatari kwa miili yetu. Anauliza, "Je, aina gani basi ya chakula kinaliwa leo na kesho na kesho kutwa?" Hapa, anamaanisha, uendelevu wa ulaji chakula kilicho salama.

Hivyo, aliamua kufanya kilimo hai kwani ndio jibu kwa mahitaji yake. Kwanza, alitengeneza mbolea ya mboji katika eneo karibu na shamba. Pili, aliamua kufanya kilimo hai katika eneo dogo la wazi na kwenye kitalunyumba (greenhouse).

Kwenye maeneo hayo anazalisha mbogamboga tofauti kama vile karoti, spinachi, mbilinganya, chainizi pokchoi, maharage, nyanya, ndizi na hata bidhaa za viungo. Lengo la kuzalisha mazao haya zaidi ni kwa matumizi ya familia na kuuza ya ziada.

## Changamoto

Moja ya changamoto anayokumbana nayo ni wadudu wanaoshambulia mboga pamoja na magonjwa hasa katika eneo la uzalishaji la wazi. Lakini, kupitia jarida la Mkulima Mbunifu na ushauri wa wataalamu mbalimbali ameweza kujifunza jinsi ya kudhibiti wadudu waharibifu pia magonjwa kwenye mimea. Anatumia madawa ya asili na kuhakikisha kwamba udongo ni wenye rutuba ya juu ili kuwa na mimea yenye nguvu na afya.

## Faida

Mama Mangalu anaeleza kuwa, kupitia kilimo hai, ameweza kutengeneza marafiki wengi ambao kwake wamemhamasisha zaidi katika kufanya mradi wa kilimo hai. Wengine wamempa ushauri juu ya soko, wengine amewashirikisha juu ya changamoto, kuweza kujadili kwa pamoja na kupata suluhisho. Wakati mwingine wanafanya majaribio na kushirikishana matokeo. Hii imekua njia ya kujifunza kadri anavyotekeleza na kusimamia mradi. Zaidi amekuwa na jambo la kumfanya awe imara zaidi kwani kila akiamka ana kazi ya kufanya.

## Funzo

"Kabla ya kuanza mradi huna budi kuondoa hofu ambayo huwapata watu wengi na kudumaza hatua muhimu za kwanza. Ni vizuri kutafuta uzoefu kutoka kwa watu wengine wanoafanya mradi kama huo wako na hata wataalamu kwa ushauri ili uweze kujitayarisha vyema kwa changamoto zozote zinazoweza kutokea kwani hazikwepeki, ila zinatatuliwa na mradi kusonga mbele".





# Fursa ya kibiashara kwa misingi ya Kilimo hai

***"Mimi ni mkulima wa mfano, ninazalisha mazao mbalimbali kwa misingi ya kilimo hai na nimefaidika sana". Hayo ni maneno ya mkulima wa kilimo hai, Bw. Michael Laizer (73), toka Kijiji cha Emaoi, Ngaramtoni, mkoani Arusha ambaye anajishughulisha na uzalishaji wa mazao ya biashara kwa misingi ya kilimo hai.***

**Flora Laanyuni**

Bw. Laizer, ambaye jina la kibiashara linalotambulika kama nembo kwenye bidhaa zake likiwa ni kilimo hai. Anaeleza kuwa, watu wengi wamezoea kilimo hai kama ni kiilimo kinachoweza kufanyika tu katika eneo dogo hasa la bustani, na kwamba haiwezekani kufanya kilimo hai katika maeneo makubwa na kama kilimo biashara

Bwana Laizer alieleza kwamba alifanya kazi SIDO kuanzia mwaka 1980 hadi 1994 na akarudi tena 2012 hadi 2019. nilipostaafu. Mnamo mwaka 2020 niliamua kujiajiri mwenyewe kwa kuanza kilimo hai bila kushawishiwa na mtu yeyote

## Kwanini kilimo hai

Laizer mwenye mke mmoja na watoto 2 anasema kuwa, aliamua kuingia kwenye kilimo hai kwasababu yuko alivyo kutokana na anachokula (I am what I eat). Hivyo akaona ni vyema kuzalisha chakula bora na salama kwa ajili yake na familia yake.

"Mbali na kuangalia afya yangu, nilikuwa nikisikia watu wakihangaika sana kutafuta mazao ya kitunguu na tangawizi na wengine wakidai kuwa kilimo cha mazao haya hakiwezekani kwa maeneo ya Arusha. Hivyo nikaamua kuwaonyesha kuwa hiyo ni fursa na kila kitu kinawezekana kikubwa tu ni kuamua''.

## Alianzaje kilimohai

Bw. Laizer anasema, alitafuta elimu ya kilimo hai kwakua ni msomi alikuwa akifahamu kuwa chanzo kikuu cha kilimo hai ni mbolea hivyo alikuwa na uhakika wa kupata mbolea ya samadi jambo lililomtia hamasa na kuamua kuanza moja kwa moja kuzalisha.

## Nini cha kuzingatia katika shamba la kilimo hai

Bwa. Laizer anaeleza kuwa, ili kufanya kilimo hai kwa ufanisi, kuna mambo muhimu ni lazima kuhakikisha unafuata ili kupata tija katika uzalishaji. Mambo hayo ni kama ifuatavyo;

- Hakikisha mfumo wa uzalishaji wa mazao yako yatazingatia kupatikana kwa chakula bora na salama. Usitumie kemikali za viwandani kuzalisha mazao ya kilimo hai.
- Urutubishaji wa udongo. Chakula kinatoka katika udongo wenye rutuba hivyo, hakikisha shamba lako linakuwa na mbolea wakati wote yaani kuwe na samadi au mboji au mbolea ya chai.
- Ni lazima uzalishe kwa kulenga soko ili kila unapovuna upeleke mazao sokoni yasiharibike.
- Fahamu kuhusu uhifadhi wa mazao mara baada ya kuvuna. Ni muhimu kujua kama ukivuna unatakiwa kuyahifadhi vipi na katika usalama kabla ya kupeleka sokoni. Ikiwa hayataenda sokoni kwa wakati huo utayatunza vipi ama utayafanyia usindikaji.

## Mazao ya kilimo hai anayozalisha na soko

Bw. Laizer anazalisha maharage machanga (green beans) kwa mkataba na shirika la Home Fresh, ambapo zao hili linavunwa kila baada ya siku tatu na kusafirishwa kwenda nje ya nchi. Pia anazalisha mapapai, vitunguu maji, vitunguu swaumu, ndizi, tangawizi pamoja na kusindika bidhaa mbalimbali kama vile, chai masala, pilau masala, tanagawizi, na asali.

## Soko la ndani

Aidha, mazao haya pia huyavuna na kupeleka kwenye soko la bidhaa za kilimo hai Mesula ambalo lipo Arusha, maeneo ya Gymkhana.

## Vipi kuhusu mkulima mbunifu

Jarida hili limekuwa tunu sana kwangu kwani nimejifunza vitu vingi ikiwa kunijengea uwezo mkubwa wa ni kwa namna gani niwashauri wakulima kuingia kwenye kilimo hai.

"Kupitia jarida majarida ya MkM nimeweza kujifunza hatua za kufuata wakati wa kufanya kilimo hai, kanuni za msingi za kilimo hai na hivyo kuniongezea wigo mkubwa katika uzalishaji wa chakula bora na salama (Toleo la 119, Agosti 2022)''.

## Wakulima wataaminije kuwa unazalisha bidhaa za kilimo hai

"Nilipoanza tu kujiingiza katika uzalishaji wa mazao ya kilimo hai, niliweza kutembelewa na waidhinishaji wa bidhaa za kilimo hai nchini Tanzania (TOAM). Wao walifanya ukaguzi na upimaji na kuidhinisha kwa kunipa cheti cha mzalishaji wa bidhaa za kilimo hai.

Pia, bidhaa zangu zimeweza kupimwa, kuidhinishwa na kupewa nembo na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuwa ni bidha salama kwa afya ya walaji''.

## Wito kwa wakulima

Kila kitu kinawezekana pale tu ukiamua kufanya. Ninawashauri wakulima kujikita katika uzalishaji wa mazao na bidhaa za kilimo hai hasa kuifanya kama kilimobiashara kwani kinawezekana na kinalipa.



# Zingatia Lishe sahihi na mifumo endelevu ya uzalishaji wa chakula salama

***Tunapozungumzia lishe tunamaanisha kupata kiasi na ubora wa chakula na maji kwa vipindi vinavyofaa ili kuruhusu mwili kufanya kazi vizuri "balanced diet" yaani mlo kamili.***

**Flora Laanyuni**

Mahitaji ya lishe hutofautiana kulingana na jinsia, umri, shughuli za kila siku, ujauzito/kunyonyesha na hali ya afya ya mtu binafsi.

Chakula kinapovunjwa, hutoa nishati ya kujenga mwili na kuupa kinga. Nishati hupimwa kwa kilokari au kilojuli. Vyakula tofauti hutoa kiasi tofauti cha nishati (kilokari) kwa gramu inayotumiwa. Nishati hii huupa mwili joto na hutumika kuruhusu seli za mwili kufanya kazi.

## Chakula

Kula ni kitendo cha kiumbe hai kuingiza chakula ndani ya mwili wake kupitia mdomo wake. Kula humfanya kiumbe hai kuwa na nguvu. Viumbe hai wanahitaji kula ili miili yao iendelee kufanya kazi. Matatizo mbalimbali ya kiafya yanaweza kutokea kiumbe asipopata mlo kamili.

Vyakula vyenye afya kama vile mboga za majani, matunda, karanga na nafaka zisizokobolewa huwa na wingi wa lishe bora, vitamini, madini, nyuzinyuzi, protini na mafuta ya omega ni muhimu sana kwa miwili wa mwanadamu kwani unahitaji virutubisho hivi ili kufanya kazi.

Chakula hutupatia nishati na malighafi ya kufanya kazi muhimu za mwili kama vile kuondoa taka, kuzuia magonjwa na kudumisha mapigo ya moyo wako.

## Sahani ya mlo unaofaa

Sahani ya Mlo unaofaa, ambayo imebuniwa na wataalamu wa lishe kutoka Chuo Kikuu cha Afya ya Jamii, Harvard na kuhaririwa na wataalamu kutoka Harvard, ni muongozo wa mlo kamili unaofaa kwa afya, ikiwa utatumiwa kwenye sahani ya mlo.




- **Sehemu kubwa ya mlo wako uwe mbogamboga na matunda (½ ya sahani)**

Hakikisha unaweka aina mbalimbali zenye rangi tofauti. Viazi mbatata havihesabiwi kama mbogamboga katika sahani ya mlo unaofaaa kwa sababu ya madhara yake kwenye kiwango cha sukari mwilini.

- **Tumia vyakula vya nafaka isiyokobolewa (¼ ya sahani)**

Vyakula vinavyotokana na nafaka isiyokobolewa kama vile ulezi, mtama, mchele wa brown vinaathari kidogo katika kiwango cha sukari mwilini na utengenezaji wa insulini kuliko vyakula vinavyotokana na nafaka iliyokobolewa.

- **Nguvu itokanayo na protini (¼ ya sahani)**

Samaki, Kuku, maharagwe, njugu, vyote ni vyakula vinavyoleta afya kutokana na protini vinaweza kuchanganywa na kachumbari. Punguza matumizi ya nyama nyekundu na epuka nyama za kusindikwa kama bacon na soseji.

- **Mafuta yatokanayo na mimea kwa kiasi**

Chagua mafuta yanayofaa ambayo yanatokana na mimea kama vile mizeituni, soya, mahindi, alizeti, karanga na mengineyo na epuka kutumia mafuta ambayo yameganda. Kumbuka kuwa alama ya "low fat" kwenye makopo ya mafuta haimaanishi "mafuta yafaayo kwa afya"

- **Kunywa maji, kahawa au chai**

Epuka vinywaji vyenye sukari, punguza matumizi ya maziwa na vyakula vitokanavyo na maziwa mpaka mara moja au mbili kwa siku, punguza matumizi ya juisi mpaka glass ndogo moja kwa siku.

## Chakula salama na vihatarishi

Chakula salama ni uhakika kuwa chakula kikitayarishwa na kuliwa kama kilivyokusudiwa hakitaleta madhara kwa mlaji.

## Vihatarishi na vyanzo vyake

Vihatarishi vya usalama wa chakula ni vile ambavyo kwa njia moja au nyingine vinaweza kufanya chakula kisiwe salama kwa matumizi ya binadamu.

## Vihatarishi vya Kibailojia (biological hazards)

Vihatarishi hivi vinajumuisha vimelea vya magonjwa kama bakteria, virusi, minyoo (parasites) na prion (aina yap rotini ambayo huweza kuharibu protini ya kawaida kwenye ubongo na kukufanya kutokuwa sawa). Mara nyingi vinaingia katika chakula kupitia malighafi zinazotumika viwandani, mazingira ambayo chakula uandaliwa, binadamu au wanyama.

Wingi wa vimelea hivi hupunguzwa au kuondolewa kabisa wakati wa kupika au kusindika na pia kwa kudhibiti mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na uhifadhi wa chakula (usafi, joto na muda)."

## Kundi la pili vihatarishi vya Kikemikali (k).

- Hivi vinaweza kupatikana ndani ya chakula chenyewe au kuingia wakati wa uhifadhi au usindikaji. Sumu hizi zinakuwepo kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kutoa kinga dhidi ya uharibifu. Sumu zinazotumika kama kinga ni kama vile cyanide katika muhogo.
- Uchafuzi wa kemikali za sumu katika mazao ya chakula mfano sumukuvu.
- Vikolezo katika vyakula ambavyo husaidia katika usindikaji ikiwa vitaongezwa katika kiwango kisichokubalika na mabaki ya kemikali ambayo hutokana na kemikali zilizotumika kwenye kilimo, mifugo, au usafi wa sehemu za uzalishaji.
- Uchafuzi wa kemikali zilizopo kwenye kitu chochote kinachogusana na chakula (food contact materials), mfano vifungashio, vifaa vya majumbani vinavyotumika kuandaa chakula (sufuria, sahani, n.k).

## Athari zitokanazo na chakula kisichokuwa salama

### *Athari za kiafya*

Hizi huweza kujitokeza ndani ya muda mfupi (food poisoning) mfano; kuumwa tumbo, kutapika, kuhara na kuhara damu au baada ya muda mrefu mfano; kansa, upungufu wa kingamwili na udumavu kwa watoto chini ya umri wa miaka mitano (5).

### *Athari za kibiashara*

Kunaweza kutokea kukataliwa kwa bidhaa za chakula zisizo na viwango vinavyokubalika katika soko na hivyo kukosa mapato.

### *Athari za uhaba wa chakula*

Chakula kilichochafuliwa zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa hakifai kwa matumizi ya binadamu hivyo hutakiwa kuharibiwa.

Athari za kuongezeka kwa gharama za matibabu na kupungua kwa nguvu kazi

Uzalishaji mali hupungua kutokana na watu wengi kuwa wanaumwa na ndugu wa karibu kutumia muda mwingi kuwahudumia.

## Nini kifanyike ili chakula kiwe salama

- Ili kuwa na chakula salama, unatakiwa mfumo thabiti wa usimamizi na udhibiti wa uzalishaji, usindikaji, usambazaji na uhifadhi wa chakula.
- Lengo kuu la kuwa na mfumo imara wa chakula salama ni kujenga mazingira ambayo yatatoa uhakika wa uzalishaji chakula ambacho ni salama ili kulinda afya ya mlaji na kukuza biashara.
- Misingi imara ya usimamizi wa usalama inahusisha mambo yafuatayo; uwepo wa sheria, muundo wa kitaasisi (usimamizi), mfumo wa ukaguzi na ufuatiliaji, huduma za maabara na elimu kwa umma.




## Mifumo endelevu ya chakula

Ni mfumo wa chakula unaotoa usalama wa chakula na lishe kwa wote kwa njia ambayo misingi ya kiuchumi, kijamii na kimazingira katika uzalishaji hauwezi kuathiri usalama wa chakula na lishe kwa vizazi vijavyo.

Kimazingira: Ni mfumo unaolinda viumbe hai, rutuba ya udongo, wanyama na mimea.

Kijamii: Ni mfumo unaolinda haki ya mwanadamu, afya na lishe. Unajali usawa wa kijinsia, tamaduni na makundi yote katika jamii.

Kiuchumi: Ni mfumo unaolinda uzalishaji wenye tija, na wenye kutoa ajira endelevu.

Kwa ujumla wake, mfumo huu hupelekea kupatikana kwa vyakula vinavyokubalika kitamaduni, kiuchumi vikiwa vya bei rafiki kwa wote, vyakula salama, na vyenye afya kwa njia ambayo inatoa usawa kwa mazingira na ustawi wa jamii.

## Kwanini kubadili mifumo yetu ya sasa ya chakula

Kuna sababu kadhaa za kushindwa kwa mifumo yetu ya chakula kwa sasa;

- Mifumo yetu ya sasa ya chakula kutokuwa na uwezo wa kuzalisha kiasi kikubwa cha chakula ili kulisha idadi kubwa ya watu duniani inayoongezeka siku kwa siku.
- Mifumo yetu ya sasa na uwezo wa kukidhi mahitaji ya lishe
- Mifumo yetu ya chakula kutokuwa na uwezo wa kumnufaisha kila mtu kwa usawa.
- Kuongezeka kwa athari hasi za mifumo ya chakula kwa mazingira na maliasili.

Jumla ya yote ni mabadiliko ya tabia ya nchi yanayozidi kuathiri mifumo ya chakula na wakati mifumo yenyewe inaendelea kuchangia kuwepo kwa mabadiliko haya.

Inakadiriwa kuwa, kati ya mwaka 2017-2019 watanzania takribani milioni 13 hawakua na chakula cha kutosha (Severely food insecure (WFP 2021) na asilimia 49% ya watanzania wanaishi chini ya dola 1.90 kwa siku (World Bank 2019).

## Tunabadilisha mifumo yetu ya chakula ili;

- Kuwa na uhakika wa chakula, afya na lishe.
- Kubadili hali ya maisha kwa wakulima. Kilimo kinaajiri watu wengi hivyo ni lazima kujali hali zao za kimaisha.
- Kuzuia uharibifu mkubwa wa mazingira, viumbe hai na baiyoanuai.

## Tufanye nini ili kubadili mifumo ya chakula

- Tunahitaji mbinu jumuishi ya mifumo ya chakula.
- Tunahitaji kufikiria zaidi ya mavuno ili kufahamu ugumu wa mifumo ya chakula.

***Kwa mawasiliano zaidi wasiliana na Ayesiga Buberwa (Meneja miradi kutoka shirika la Iles De paix- IDP ) kwa simu namba 0762 542 253***

# Usindikaji na mnyororo wa thamani husaidia kumnyanyua mkulima kiuchumi

***Mara nyingi wakulima na wafugaji hufanya kazi zao kwa bidii na kuzalisha kwa wingi, lakini kumekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuwa hawapati faida kutokana na mazao yao kununuliwa kwa bei ambayo haikidhi hata gharama walizotumia kuzalisha.***

**Ayubu Nnko**

Ili kuondokana na hali hii ni lazima wakulima na wafugaji kubadili mtazamo wao na namna wanavyofanya kazi zao. Moja wapo ya njia ambazo wanaweza kubadili ni kuhakikisha kuwa wanatafuta masoko kwa ajili ya mazao yao, lakini pia kuhakikisha kuwa wanaongeza mazao yao thamani na wasiuze yakiwa ghafi. Hii inaweza kufanyika kwa kusindika na kufungasha, kisha kupeleka sokoni wao wenyewe

Tanzania ina uwezo wa kuzalisha chakula kukidhi mahitaji ya taifa kwa zaidi ya asilimia 100. Inakadiriwa kuwa asilimia 30 hadi 40 ya kiasi cha nafaka kinachozalishwa nchini kila mwaka hupotea bila kutumiwa na walaji. Aidha, upotevu huu ni mkubwa zaidi kwa mazao yanayoharibika haraka kama vile mazao ya mizizi, mbogamboga na matunda.



Picha:MkM

### Ili kudhibiti hali hii ni muhimu mambo matatu yakazingatiwa.

- Kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvuna kwa kuyaweka katika minyororo ya thamani ya bidhaa, inayowanufaisha wadau na kuchangia katika kuwa na uhakika wa chakula, lishe na ukuaji wa uchumi.
- Kuboresha usimamizi wa mazao baada ya kuvuna kwa kuhakikisha uwepo wa mbinu na teknolojia za kupunguza upotevu na kuongeza thamani ya mazao baada ya kuvuna.
- Kutoa motisha kwa uwekezaji katika mifumo ya masoko, pamoja na kuboresha uwezo wa uratibu wa mkakati wa kuongeza mazao thamani.



Picha:IN

Usindikaji unasaidia kuepuka upotevu wa aina mbalimbalimbali kama ifuatavyo;

Kiasi cha Upotevu wa mazao -Hii ni aina ya upotevu unatokana na kupungua kwa kiasi halisi cha mazao.

Upotevu wa ubora – Hii inahusisha upotevu wa sifa za mazao kama vile umbo, ukubwa, rangi, ladha na viru tubisho.

Upotevu wa kiuchumi/thamani au kibiashara – Kuporomoka thamani ya kifedha ya mazao katika soko unaotokana na zao husika kupoteza viwango vya ubora au kiasi.

### Usindikaji

Usindikaji ni mchakato au kitendo cha kuweka mazao katika namna maalumu ili yakae kwa muda mrefu bila kuharibika. Kuna aina nyingi ya mazao yatokanayo na mimea na Wanyama yanavyoweza kusindikwa. Kwa mfano: Mbogamboga, nyama, samaki, maziwa, matunda ya aina mbalimbali kama vile zabibu, maembe, machungwa, parachichi, mahindi mtama na kadhalika.

Mazao hayo hutumika katika kutengenezea bidhaa mbalimbali kama vile juisi za matunda, nyama za viwandani (za vikopo) n.k.

Tafiti zinaonesha kuwa wakulima wa mazao yanayoharibika haraka kama vile mazao ya matunda, wamekuwa wakipata hasara kubwa pindi soko linapoyumba hivyo kuwasababisha kuwa duni na kukosa kuwa na uzalishaji endelevu.

Wazalishaji wa mazao ya matunda kama vile nyanya, embe, parachichi na mengineyo wanawezakufanya usindikaji na kupata bidhaa kamili ambayo itadumu kwa muda mrefu, lakini pia kuwaongezea pato.

Kwa Mfano, wazalishaji wa nyanya mkulima anaweza kuongeza thamani zao hilo kwa kutengeneza bidhaa kama vile mvinyo, tomato source, chachandu nakadharika.

Badala ya mkulima kuacha nyanya zake zioze kwa kukosa bei anaweza kuchukua hatua ya kusindika nyanya hizo ili kupata mvinyo, ambayo anawezakuuza chupa moja kati ya fedha za kitanzania 12000-15000, jambo ambalo litamuongezea pato badala ya kupata hasara.

Hali kadhalika bidhaa nyingine zinazotokana na zao hilo zinaweza kumuinua mkulima kuliko kuacha zao likioza kwa kigezo cha bei au kutokuwa na soko msimu huo.

(Unaweza kujifunza zaidi namna ya usindikaji wa nyanya kupata mvinyo kutoka jarida la MkM Toleo la 20, la mwaka 2014).



Picha:MkM





# Muhimu kufikiria mnyororo wa thamani katika mazao ya kilimo hai na Ufugaji

***Ukiwa kama mkulima ama mfugaji, wewe ni mjasiriamali, bila shaka ungependa kunufaika na mazao yako. Hivyo ni muhimu kufikiria kuhusu mnyororo wa thamani kwa mazao unaozalisha ili kuongeza tija.***

**Dorothea Chambo**

### Mnyororo wa thamani

Mnyororo wa thamani (value chain) ni mfumo mzima wa uzalishaji, usindikaji na uuzaji wa bidhaa za kilimo na mifugo, tangu mwanzo wake hadi bidhaa hiyo itakapokuwa tayari kuliwa na mlaji wa mwisho. Mnyororo wa thamani hujumuisha wahusika mbalimbali wanaounganishwa na mtiririko wa bidhaa, fedha, taarifa na huduma.

Kadri mazao ya kilimo na mifugo yanavyopitia hatua kadhaa za mnyororo wa thamani ndivyo thamani yake inavyozidi kuongezeka.

Katika kila hatua ya mnyororo wa thamani, thamani ya bidhaa husika huzidi kuongezeka kwa sababu bidhaa hii huwa rahisi zaidi kwa mteja kuweza kuitumia.

Pia thamani ya bidhaa pamoja na bei huongezeka katika kila kiwango kwenye mnyororo huu.

### Hatua za kufuata katika mnyororo wa thamani

Mnyororo wa thamani hujumuisha kazi mbalimbali kama vile uzalishaji, usafirishaji, usindikaji, uhifadhi, upangaji wa madaraja, kufungasha na masoko.

### Uzalishaji

Kazi hii hufanyika kwa kufuata taratibu zote za uzalishaji wa mazao kwa kufuata kanuni na taratibu zote za uzalishaji wa zao husika. Hii ni pamoja na kutumia mbegu sahihi, kupanda kwa wakati, matunzo sahihi, kwa kufuata kanuni zote muhimu katika kilimo hai, ikiwa ni pamoja na kutotumia kemikali na kuzingatia utunzaji wa mazingira.

### Usafirishaji

Hii ni moja ya hatua muhimu katika mnyororo wa thamani, kwa kuwa lengo lake ni kusogeza bidhaa kwa mlaji na kurahisisha huduma. Hatua pia huongeza thamani, na ndiyo sababu bei ya shambani hutofautiana na bei ya sokoni.

Ni muhimu kwa wasafirishaji kuzingatia kanuni husika ili bidhaa ifike sokoni ikiwa bado na ubora unaostahili.

### Uhifadhi

Ni muhimu wakulima kuhakikisha kuwa wana utaratibu mzuri wa kuhifadhi mazao yao kunapokuwa na mazao mengi. Mkulima ajifunze njia mbalimbali za uhifadhi kwa matumizi ya baadae. Mfano ukaushaji wa matunda.

Uhifadhi husaidia upatikanaji wa zao au bidhaa husika katika kipindi ambacho yasingepatikana. Ni muhimu kuzingatia kanuni sahihi za uhifadhi bila kutumia kemikali.

Zingatia usafi wa mazingira na viwango vinavyokubalika. Usipohifadhi kwa usahihi ni rahisi kushusha thamani ya mazao husika.

### Upangaji katika madaraja

Hii ni moja ya hatua muhimu sana, ambayo humsaidia mkulima au mzalishaji kupata bei tofauti kwa mazao au bidhaa aliyozalisha. Hii ni kwa sababu mazao yenye ubora zaidi ni rahisi kuuzika kwa bei ya juu, kuliko yale ambayo yana ubora hafifu. Mkulima anaweza kupanga bei awezavyo kulingana na madaraja na ubora wa bidhaa zake.



Picha:IN

### Usindikaji

Hii ni hali ya kubadili bidhaa yako kutoka katika hali moja na kuwa na thamani Zaidi. Ni mwanzo wa kufanya bidhaa kuwa na maisha marefu Zaidi.

Mfano ni ukaushaji wa mbogamboga na matunda kwa matumizi ya baadae. Hali hii hutoa fursa ya bei zaidi kwa bidhaa husika na ajira kwa watakaojumuishwa katika kazi hiyo.

### Ufungashaji

Hii ni hatua inayofuata baada ya usindikaji. Shughuli hii hujumuisha ufungashaji katika viwango tofauti. Hii inasaidia walaji wenye uwezo na uhitaji tofauti kuweza kupata huduma hiyo. Pia hali hii husaidia kuweka bidhaa katika hali ya kuwa na umbo sahihi na kuvutia.

Hatua hii ni hujumuisha vipimo na viwango vinavyokubalika kimataifa. Hii ni pamoja na uwekaji wa nembo yenye taarifa sahihi.

### Soko

Hii ni hatua ya mwisho kabisa katika mnyororo wa thamani. Hapa muuzaji na mnunuzi hukutana na kufanya biashara. Soko la bidhaa unazozalisha itategemea ni jinsi gani ulivyozingatia hatua zote muhimu kama ilivyoelezwa katika maelezo na hatua za awali.

Uuzaji katika soko pia hutegemea sanaa ya muuzaji ikiwa ni pamoja na kuifahamu vizuri bidhaa yake. Kwa mfano; Muuzaji wa bidhaa za kilimo hai ni lazima aelewe na kueleza kwa ufasaha kabisa upekee uliopo katika bidhaa zinazotokana na kilimo hai.

Unaweza kuongeza thamani ya bidhaa zako kwa kuweka walaji katika madaraja, kutangaza bidhaa zako, pamoja na ulinganifu wa uwezo wa kununua.

**Muhimu:** Usafi ni nguzo muhimu katika mnyororo wa thamani. Zingatia usafi wa bidhaa na mazingira wakati wote. Badili muonekano wa eneo na bidhaa kila wakati.

Ni vyema kukumbuka na kuzingatia kuwa kila anaeshiriki katika hatua moja wapo, huongeza thamani na hivyo kuvutia ongezeko la gharama, hivyo ni muhimu kufikiri namna nzuri na bora inayoweza kufupisha mnyororo, ili usiwe mrefu sana na kusababisha bei ya bidhaa kuwa kubwa sana.

### Changamoto

- Umakini wa hali ya juu unahitajika katika kulinda ubora wa mazao ya kilimo hai, ili kutokuchanganya bidhaa zako na zile zilizozalishwa kwa kutumia kemikali.
- Kuna changamoto kubwa kwa usafirishaji, kwa wanaosafirisha kutoka vijijini, kwani mara nyingi huishia kuchanganya mazao yao na yale yaliyozalishwa kwa kutumia kemikali.

***Kwa maelezo Zaidi juu ya mnyororo wa ongezeko la thamani, unaweza kuwasiliana na shirika la kilimo endelevu SAT kwa namba 0754925560***

# Sikiliza vipindi vya kilimo ikolojia

Kama ilivyo ada *Mkulima Mbunifu* imeendelea kushirikiana na wadau wengine kuhakikisha inakufikishia taarifa sahihi za kilimo hai. Kwa mantiki hiyo, usiache kusikiliza vipindi vya kilimo hai vinavyoletwa kwako na shirika la Farm Radio International kupitia stesheni mbalimbali za radio.



| JINA LA RADIO | JINA LA KIPINDI | NAMBA YA KUBIPU | SIKU YA KIPINDI | | MARUDIO YA KIPINDI | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | SIKU | MUDA | SIKU | MUDA |
| RADIO MWANGAZA | KILIMO NA MWANGAZA | 784105727 | IJUMAA | 2:30-3:00 USIKU | JUMATATU | 2:30-3:00 USIKU |
| RADIO STANDARD FM | KILIMO NA JAMII | 784105733 | JUMAMOSI | 1:00-1:30 JIONI | JUMATANO | 1:30-2:00 USIKU |
| RADIO UTUME | KILIMO NA MKULIMA | 784105788 | ALHAMISI | 2:30-3:00 USIKU | JUMAPILI | 1:00-1:30 JIONI |
| RADIO HABARI NJEMA | JUKWAA LA MKULIMA | 784105711 | JUMAMOSI | 3:00-3:30 USIKU | JUMATANO | 3:00-3:30 USIKU |
| RADIO SAUTI YA INJILI | JICHO LA MKULIMA | 784105718 | JUMAMOSI | 1:30-2:00 USIKU | JUMATANO | 12:00-12:30 JIONI |

# Soko la mazao ya kilimo hai Tanzania

***Ingawa taasisi nyingi zinasisitiza kilimo hai nchini Tanzania, kuna walaji wachache sana walio na uelewa wa bidhaa za kilimo hai. Soko la mazao ya kilimo hai lipo tu na kufahamika katika miji mikubwa kama vile Dar es Salaam na Arusha, na mashirika machache yaliyoidhinishwa katika kuuza mazao kwa misingi ya kilimo hai kwa ajili ya soko la ndani na hata nje.***

**Flora Laanyuni**

## Uuzaji nje bidhaa za kilimo hai na usajili

Kwa kawaida soko la nje la bidhaa za kilimo hai huhitaji usajili na nembo kwenye bidhaa. Kwa usajili, kampuni inayojitegemea ni lazima iwadhibiti wazalishaji (kwa kawaida mwaka mmoja) ili kudhibitisha kuwa bidhaa hiyo imezalishwa kwa kufuata misingi na vigezo vya kilimo hai. Vigezo vinaelezea kwa undani ni kwa namna gani bidhaa inaweza kuzalishwa, kuwekwa nembo na kuuzwa kama bidhaa ya kilimo hai.

Mfano, nchini Tanzania, Tanzania Organic Agriculture Movement (TOAM) ndilo linalothibitisha bidhaa za kilimo hai ambazo huzalishwa na kuuzwa nchini n ahata nje ya nchi.

Usajili na kuweka nembo unahakikisha kuwa si kila mzalishaji anaweza kudai kuwa bidhaa yake imezalishwa kwa kufuata kilimo hai. Nembo husaidia kutoa uhakika kuwa ni kweli bidhaa husika imezalishwa kwa kuzingatia mfumo wa kilimo hai. Kama umempata mnunuzi wa bidhaa za kilimo hai ni lazima ufuate masharti na kanuni halisi za uzalishaji hai.

Orodha ya mahitaji ni kubwa na inaweza kuwa tofauti na ile inayofuatwa katika kilimo cha jadi na kilimo cha kisasa. Unachohitajika ni kufahamu mahitaji halisi na vigezo, mfano: - ni dawa zipi zinazohitajika kutumima kudhibiti wadudu na magonjwa, uzalishaji, uhifadhi na vifungashio vya bidhaa vinavyotakiwa. Udhibiti na usajili hugharamiwa na mkulima mwenyewe.

Mafunzo ni muhimu kwa ajili ya uzalishaji uliosajiliwa



Picha:IN

Ni changamoto kwa wakulima wadogo wadogo kuondokana na kilimo cha kisasa na kuingia katika kilimo hai. Baadhi ya mashirika yamekuwa yakiingia mikataba na wakulima kwa ajili ya kuzalisha kwa kuzingatia misingi ya kilimo hai, kisha kununua kwa ajili ya kuuza nje, na kwa kawaida huwapatia mafunzo. Kwa sababu ya gharama kubwa za kupata usajili, wakulima wadogo ni lazima wajiunge katika vikundi vya wazalishaji. Kwa misingi hii, gharama za usajili zitagawanywa kwao na hii itawapa unafuu mkubwa sana.

## Soko la nyumbani la mazao ya kilimo hai

Masoko machache ya ndani yasiyo rasmi, taasisi n.k, mara nyingi hayahitaji usajili, na badala yake yanaweza kutegemea gharama ndogo kutambulika. Kwenye miji mikubwa, kuna nafasi kubwa ya kupata soko la bidhaa za kilimo hai.

Kuna mifano mingi ya mafanikio katika kuanzisha soko la bidhaa za kilimo hai. Kwa kutumia usajili na nembo, mlaji anaweza kushawishiwa na uhalisia wa bidhaa za kilimo hai. Kuna mashirika mengi ambayo kwa sasa yanajihusisha na kilimo hai, ikiwa ni pamoja na vikundi vya vijana. Kila siku vijana wamekuwa wakiweka mboga na bidhaa nyingine katika mashamba yao kwenye meza na kisha kuwaelewesha na kuwafundisha wanunuzi ni kwa jinsi gani hizo bidhaa zina ubora wa hali ya juu. Ni kwa nini wewe usiwafuate ukawa mfano wa kuigwa?

Kama una uhakika na unachozalisha, basi wafahamishe walaji wa ndani kuhusu bidhaa zako, ubora wake na ni kwa nini wanunue kutoka kwako. Hii inaweza kufanyika kwa mdomo tu au kwa vipeperushi. Jivunie ulicho nacho.

***Kwa maelezo zaidi Unaweza kuwasiliana na Mkulima Mbunifu kwa simu namba +255 0717266007 au kwa barua pepe info@mkulimambunifu.org***



Haki zote zimehifadhiwa ©2023 *Mkulima Mbunifu*